

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA UPIMAJI WA
DARASA LA PILI

201 STADI YA KUSOMA

Muda: Dakika 15 Ijumaa, 12 Aprili 2019 asubuhi

Maelekezo

- 1. Karatasi hii ina maswali matatu (3).**
- 2. Mwanafunzi anatakiwa kujibu maswali yote kwa mdomo.**
- 3. Kila mwanafunzi atapimwa kwa dakika 15.**
- 4. Msimamizi anatakiwa kujaza taarifa za mwanafunzi katika nafasi zilizo wazi juu ya fomu maalum ya upimaji kwa kalamu ya wino wa bluu.**
- 5. Mwanafunzi atakapokuwa amemaliza kusoma, msimamizi anatakiwa kujaza alama katika fomumaalum ya upimaji kwa kutumia kalamu ya wino mwekundu.**

Kusoma Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.*
- (ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.*
- (iii) Hakikisha mwanafunzi anatumia **sekunde tatu tu**, kusoma kila neno. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.*
- (iv) Usomaji wa maneno utafanyika kwa **dakika tatu**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika mbili** zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya upimaji.*

1. Mwanafunzi asome maneno yafuatayo:

televisheni gita vitamini wiki picha

kompyuta pini mdomo sentensi nyumba

tochi Baiskeli mwanafunzi ubao mwavuli

chumvi saa mbwa mwezi kikombe

mchele mkono mwanga karoti jogoo

Kusoma Sentensi

Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi kwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwakalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.*
- (ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma sentensi kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.*
- (iii) Hakikisha mwanafunzi anatumia **sekunde tatu tu**, kusoma neno katika **sentensi**. Baada ya sekunde **tatu** mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.*
- (iv) Usomaji wa sentensi zote utafanyika kwa **dakika nne**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika tatu** zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya upimaji.*

2. *Mwanafunzi asome sentensi zifuatazo:*

- (i) Mbuzi wangu wana mikia mifupi.*
- (ii) Njoo hapa dada yangu mpole.*
- (iii) Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.*
- (iv) Viatu vyangu vyote ni vyeusi.*

(v) *Hawa ni watoto wadogo sana.*

Kusoma Kifungu cha Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Mwoneshe mwanafunzi kifungu cha maneno (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari na mweleze mwanafunzi kuwa akimaliza kusoma, utachukua karatasi yake na utamuuliza maswali yanayohusiana na kifungu cha maneno alichosoma.*
- (ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika fomu maalum ya Upimaji.*
- (iii) Mwanafunzi akimaliza kusoma, chukua karatasi yake ya upimaji kisha muulize maswali yaliyopo katika fomu maalum ya Upimaji.*
- (iv) Usomaji wa kifungu cha maneno utafanyika kwa dakika nane, ambapo dakika tatu zitatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na dakika tano zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya Upimaji.*

3. *Mwanafunzi asome kifungu cha maneno kifuatacho kisha ajibu maswali atakayoulizwa na msimamizi kwa mdomo:*

Furaha ana umri wa miaka nane. Anaishi Kinondoni na kaka yake mkubwa. Mara zote hutunza vitu vyake vizuri. Siku ya Jumatatu, Furaha alikwenda dukani kununua Penseli. Alikuwa na shilingi mia tano mfukoni. Alinunua penseli mbili kwa shilingi mia nne. Furaha alibaki na shilingi mia moja ambazo alizitumia kununua kifutio.